

WAZO LANGU

~~Habari Leo Jumatano Mei 13, 2026 19/6~~

Madereva ongezeni umakini kupunguza ajali za barabani



Na Rehema Lugono

USALAMA barabarani ni muhimu katika maisha ya kila siku ya wananchi ikizingatiwa kwamba barabara hutumiwa na waenda kwa miguu, madereva wa vyombo vya usafiri tofauti.

Kutokana na matumizi hayo ya pamoja, kunahitajika nidhamu, umakini na utii wa sheria ili kuhakikisha kila mtu anafika salama anapokwenda.

Hivi karibuni kume kuwa na matukio ya ajali za barabarani ikiwemo ajali iliyotokea Mei 8, mwaka huu Tanangozi mkoa wa Iringa ambapo watu watano walifariki na wengine 28 kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha basi la kampuni ya Shabiby Line na lori lililokuwa limebeba shehena ya soda.

Pia, juzi watu wawili

walifariki na wengine 13 kujeruhiwa katika ajali ya barabarani iliyotokea eneo la Mseke, Iringa baada ya basi la Kampuni ya Classic kugongana uso kwa uso na gari jingine kabla ya kupinduka na kutumbukia korongoni.

Hayo ni baadhi ya matukio ya ajali lakini yapo mengine yaliyotokea hivi karibuni ikiwemo ya mkoani Dodoma baada ya malori mawili kugongana na kuwaka moto.

Miongoni mwa sababu zinazotajwa kuchangia ajali hizo ni kuendesha gari kwa kasi bila kuzingatia hali ya barabara, hali ya hewa, au uwepo wa watumiaji wengine wa barabara.

Kuendesha gari kwa kasi kunapunguza uwezo wa dereva kufanya uamuzi maamuzi sahihi kwa wakati na kuongeza uwezekano wa kushindwa kulidhibiti gari hatari inapojitokeza.

Nashauri madereva kuzingatia sheria za barabarani ikiwamo kukagua vyombo vyao kabla ya kuanza sa-

fari ili kupunguza kuwasababishia watumiaji wengine vifo, majeraha, ulemavu wa kudumu, pamoja na hasara kubwa za kiuchumi na kijamii.

Aidha, madereva wazingatie viwango vya mwendo vilivyowekwa na mamlaka husika ili kuhakikisha usalama wa abiria na watumiaji wengine wa barabara, kuepuka matumizi ya simu wakati wa kuendesha kwa sababu huondoa umakini wa dereva na kuongeza hatari ya kupata ajali.

Madereva waelewe kuwa maisha ya watu wengi yanategemea umakini wao wanapokuwa kwenye usukani kwa sababu vifo vinasababisha taifa kupoteza nguvu kazi za taifa.

Matumizi ya pombe na dawa za kulevya ni tatizo kubwa linalochangia ajali nyingi.

Hata hivyo maafisa usalama barabarani wamekuwa wakielemba kwamba dereva aliyekunywa pombe hupoteza uwezo wa kufikiri

vizuri, kuona kwa umakini, na kufanya uamuzi sahihi.

Nashauri madereva wanaofanya safari ndefu wanapojihisi uchovu, wapumzike vya kutosha kabla ya kuanza safari.

Vilevile elimu ya usalama barabarani inapaswa kuendelea kutolewa kwa madereva wote.

Kwa upande mwingine, kila abiria ana jukumu la kuhakikisha usalama unakuwapo wakati wa safari kwa kumkemea dereva pamoja na kutoa taarifa kwa mamlaka husika pale wanapoona dereva anakiuka sheria za barabarani.

**MSAMIATI
WA LEO**

HabariLEO

Mawenge:

Hali ya kukosa utulivu wa akili

NUKUU

"Serikali ina nia ya dhati ya kuwanufaisha wananchi kutokana na rasilimali zilizopo ndani ya nchi. Kwa kufanya hivyo, tutaendelea kuwekeza katika miradi mbalimbali ya kijamii kama sehemu ya kurudisha kwa wananchi kutokana na gesi tunayoipata kuendeleza uchumi wa nchi yetu," - Naibu Waziri wa Nishati, Salome Makamba, Dodoma, Mei 11, 2026.

191